

Sheria Ndogo Za (Hifadhi ya Mazingira) Za Halmashauri ya Mji wa Kondoa

TANGAZO LA SERIKALI NA. 512 la tarehe 14/9/2018

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA MIJI)

SURA YA 288

SHERIA NDOGO

Zimetungwa chini ya kifungu cha 89

SHERIA NDOGO ZA (HIFADHI YA MAZINGIRA) ZA HALMASHAURI YA MJI WA
KONDOOA ZA MWAKA 2018

SEHEMU YA KWANZA:
UTANGULIZI

Jina na
tarehe ya
kuanza
kutumika

1. Sheria Ndogo hizi zitaitwa Sheria Ndogo za (Hifadhi ya Mazingira) za Halmashauri ya Mji wa Kondoa za Mwaka 2018 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika maeneo yote ya Halmashauri ya Mji wa Kondoa.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa pale itakapoelekezwa vinginevyo;

“Afisa Mwidhiniwa” maana yake ni Afisa ye yote wa Halmashauri atakaye teuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;

“Eneo la Hifadhi” maana yake ni maeneo ya milima, mbuga za wanyama, maeneo ya vyanzo vya maji, hifadhi ya misitu na maeneo mengine ambayo yatatangazwa na Halmashauri kuwa ni maeneo ya hifadhi;

Sheria Ndogo Za (Hifadhi ya Mazingira) Za Halmashauri ya Mji wa Kondoa
Tangazo la Serikali Na. 512 (Linaendelea.)

“*Halmashauri*” maana yake ni Halmashauri ya Mji wa Kondoa;

“*Hifadhi ya Mazingira*” maana yake ni utunzaji endelevu wa ardhi, mimea, hewa, viumbi hai na visivyo hai na vyanzo vya maji vinavyo zingatia masharti na maelekezo yatakayo tolewa na Afisa Mwidhiniwa chini ya Sheria Ndogo hizi au Sheria nyingine yoyote;

“*Kiwanda*” maana yake ni jengo, majengo au eneo ambapo vitu vinatengenezwa au kuzalishwa;

“*Kuvuna misitu*” maana yake ni kufyeka, kukata au kung’oa miti, kwa njia endelevu;

“*Maeneo ya malisho*” maana yake ni sehemu zote ambazo zimetengwa na Halmashauri au Kijiji kuwa maeneo ya Malisho ya mifugo;

“*Majii*” maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira 2004;

“*Maji taka*” maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira 2004;

“*Mazao ya misitu*” maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Misitu chini ya kifungu cha 2;

“*Mazingira*” maana yake ni kama ilivyo tafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004;

Na. 20/2004

“*Mfugaji*” maana yake ni mtu ye yeyote anayejishughulisha na ufugaji mifugo katika eneo la Halmashauri;

“*Mifugo*” maana yake ni mifugo yoyote inayofugwa na binadamu;

Sheria Ndogo Za (Hifadhi ya Mazingira) Za Halmashauri ya Mji wa Kondoa
Tangazo la Serikali Na. 512 (Linaendelea.)

“*Misitu*” maana yake ni eneo la ardhi ambalo limefunikwa angalau kwa asilimia 10 ya miti, uoto wa asili au iliyopandwa, au asilimia 50 au zaidi, ya vichaka na miti na miti inayoota upya ambayo itajumuisha aina yote ya misitu ya hifadhi ambayo itatangazwa chini ya Sheria ya Misitu Na.14 ya mwaka 2002 na mazao yote ya misitu ikijumuisha majani na nyasi ndani ya eneo la Halmashauri;

“*Taka*” maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira 2004;

“*Taka Ngumu*” maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira 2004;

“*Taka za Viwandani*” maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004;

“*Uchafu Hatari*” maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika kifungu cha 133(5) cha Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004;

“*Uchafuzi wa Mazingira*” maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004;

“*Udongo*”maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Mazingira 2004;

“*Vitu hatari*” Maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Mazingira 2004.

SEHEMU YA PILI:
MASHARTI YA UFUGAJI

Sheria Ndogo Za (Hifadhi ya Mazingira) Za Halmashauri ya Mji wa Kondoa
Tangazo la Serikali Na. 512 (Linaendelea.)

- | | | |
|---|------|--|
| Wajibu wa
mfugaji | 4. | Kila Mfugaji chini ya Sheria Ndogo hizi; |
| | | (a) atatakiwa kufuga idadi ya mifugo kama atakavyo elekezwa na Halmashauri; |
| | | (b) atatakiwa kufuga na kulisha mifugo yake katika maeneo ya malisho yaliyo pangwa na Halmashauri; |
| | | (c) atatakiwa kupitisha mifugo yake katika njia zilizopangwa na kutengwa na Halmashauri; |
| | | (d) atatakiwa kuwa na kadi ya mifugo itakayo onyesha idadi na aina ya mifugo aliyonayo; |
| | | (e) atatakiwa kupeleka mifugo katika majosho kama atakavyo agizwa na Halmashauri; |
| | | (f) atatakiwa kuweka alama kwenye mifugo yake kama itakavyo elekezwa na Halmashauri. |
| Masharti
kwa Mfugaji | 5. | Ni marufuku kwa mfugaji au mtu yeyote: |
| | | (a) kusafirisha mifugo kwa kuiswaga barabarani; |
| | | (b) kusafirisha au kuhamisha mifugo kutoka eneo moja hadi lingine bila kibali kutoka kwa Halmashauri; |
| | | (c) kuingiza mifugo katika eneo la Halmashauri bila kibali; |
| | | (d) kuuza au kununua mifugo katika maeneo ambayo siyo mnada, masoko au magilio ya mifugo yaliyo idhinishwa na Halmashauri; |
| | | (e) kufuga mifugo mingi katika eneo dogo; |
| | | (f) kuchunga, kulisha au kunywesha maji mifugo katika maeneo ambayo hayakutengwa kwa shuhguli hiyo. |
| Kudhibiti
mifugo
inayozurula
hovyo | 6(1) | Halmashauri itakamata mifugo au mfugo wowote utakao onekana unazurura hovyo au kulishwa katika maeneo yasiyo ruhusiwa katika eneo la Halmashauri |

Sheria Ndogo Za (Hifadhi ya Mazingira) Za Halmashauri ya Mji wa Kondoa
Tangazo la Serikali Na. 512 (Linaendelea.)

- (2) Endapo mwenye mifugo au mfugo hatatokea ndani ya kipindi cha siku saba (7) tangu kukamatwa kwa mifugo hiyo, Halmashauri itakuwa na uwezo wa kuza kwa mnada mfugo au mifugo hiyo baada ya kupata idhini ya Mahakama na fedha zitakazopatikana zitafidia gharama za Halmashauri na zitakazobaki zitarudishwa kwa mwenye mifugo.

SEHEMU YA TATU:
KILIMO NA UHIFADHI WA ARDHI

- Taratibu za Kilimo Sura ya 113 na 114
- 7(1) Mtu yeote atakayetaka kuendesha shughuli za kilimo katika Halmashauri atatakiwa kuzingatia taratibu za kilimo kwa kuzingatia Kalenda ya Kilimo ya Halmashauri na kwa kuzingatia Sheria ya Ardhi na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira.
- (2) Itakuwa halali kwa Halmashauri kuingia katika shamba lolote kwa madhumuni ya kufanya ukaguzi na kuhakikisha utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.
- Masharti kwa Mkulima
8. Itakuwa ni marufuku kwa Mtu yeote;
- (1) kulima katika miteremko, karibu na vyanzo vyta maji, kandokando ya mito, Mabwawa na maziwa au kufanya jambo lolote litakalo haribu hifadhi ya mazingira.
- (2) kutumia ardhi kinyume na matumizi kama ilivyopangwa na kuidhinishwa na Halmashauri.
- (3) kusafisha shamba kwa njia ya kuchoma moto, isipokuwa kwa kibali maalumu kutoka Halmashauri.
- (4) kuchimba mchanga katika maeneo yasiyo ruhusiwa kama vile maeneo ya makazi ya watu, maeneo ya hifadhi, kandokando ya mito au ndani ya mto, bwawa au ziwa

Sheria Ndogo Za (Hifadhi ya Mazingira) Za Halmashauri ya Mji wa Kondoa
Tangazo la Serikali Na. 512 (Linaendelea.)

isipokuwa kwa ruhusa maalumu ya Halmashauri.

(5) kuchimba Mawe, Udongo, Mchanga, Kokoto zaidi ya mita tatu kuelekea chini ya Ardhi.

Kibali cha
kuchoma
moto

9. (1) Itakuwa ni marufuku kwa mtu yejote kusafisha shamba kwa kuchoma moto isipokuwa kwa kibali cha Halmashauri.

(2) Kibali kitakachotolewa chini ya Sheria Ndogo hizi kitakuwa cha maandishi na kitaonesha jina la mwenye kibali, tarehe na eneo analotaka kuchoma moto.

(3) Muda unaoruhusiwa kuchoma moto chini ya Sheria Ndogo hizi ni kuanzia saa 12:00 Asubuhi hadi saa 4:00 asubuhi na saa 12.00 jioni hadi saa 1.00 jioni.

Uhifadhi wa
Ardhi

10. Itakuwa ni wajibu wa wakazi wa eneo ambalo uoto wa asili au mazingira yameharibiwa, kuhakikisha kuwa wanalirudisha katika hali yake ya kawaida kwa kupanda miti na kuendelea kutoharibu mazingira ili kuwezesha uoto urudi katika hali yake ya kawaida.

Ujenzi
Holela

11. Mtu yejote hataruhusiwa kujenga nyumba au jengo lolote katika eneo ambalo Halmashauri imetangaza kuwa eneo la Hifadhi.

SEHEMU YA NNE:
HIFADHI YA VYANZO VYA MAJI

Wajibu wa
Kulinda
Vyanzo vya
Maji

12. (1) Itakuwa ni wajibu wa kila mtu ndani ya Halmashauri kupanda miti isiyonyonya maji kwa kuzingatia maelekezo ya Afisa Misitu.

(2) Ni marufuku kwa mtu yejote kuishi, kulima, kukata miti, kuchunga mifugo au kufanya jambo lolote linaloharibu

Sheria Ndogo Za (Hifadhi ya Mazingira) Za Halmashauri ya Mji wa Kondoa
Tangazo la Serikali Na. 512 (Linaendelea.)

kwa namna yoyote eneo lilitotangazwa kuwa eneo la hifadhi au chanzo cha maji.

- (4) Ni marufuku kwa mtu ye yoyote kumiliki chanzo cha maji kilichopo ndani ya Halmashauri.

Uchafu wa vyanzo vya maji 13. Itakuwa ni kosa chini ya Sheria Ndogo hizi kwa mtu ye yoyote kuelekeza mabomba ya maji machafu kwenye mito, mabwawa, ziwa, visima, mifereji, chemchem au sehemu yoyote ambayo ni chanzo cha maji.

SEHEMU YA TANO:
UHIFADHI WA MISITU

Kuchoma au kusababisha moto 14. (1) Mtu ye yoyote hataruhusiwa kukata miti katika maeneo ya misitu iliyohifadhiwa kwa ajili ya matumizi ya aina yoyote bila kupata kibali kutoka Halmashauri.

- (2) Mtu ye yoyote hataruhusiwa kuchoma moto misitu kwa namna yoyote ile katika misitu iliyoko eneo la Halmashauri.

(3) Iwapo moto utatokea katika eneo la Halmashauri na ukaonekana kuwa na madhara kwa maisha, mali za watu na uharibifu wa mazingira katika eneo husika, kiongozi wa eneo husika atawajibika kutoa amri kwa wakazi wa eneo hilo kwenda kuzima moto huo.

- (4) Kila mkazi wa eneo hilo atawajibika kushiriki katika zoezi la kuzima moto huo endapo atatakiwa kufanya hivyo, kama atashindwa kushiriki katika kuzima moto bila sababu ya msingi atakuwa ametenda kosa.

Ukataji miti 15. (1) Itakuwa ni kosa chini ya Sheria Ndogo hizi kwa mtu ye yoyote kuvuna miti pasipo kuwa na kibali cha uvunaji wa miti.

Sheria Ndogo Za (Hifadhi ya Mazingira) Za Halmashauri ya Mji wa Kondoa
Tangazo la Serikali Na. 512 (Linaendelea.)

(2) Afisa misitu atatakiwa kuhakikisha kama miti inayovunwa imekomaa na inafaa kwa ajili ya matumizi.

(3) Watu wanao vuna miti kwa ajili ya kuchoma mkaa, watatakiwa kuwa na eneo maalum lililoidhinishwa na Afisa misitu kwa ajili ya kuchomea mkaa huo.

(4) Ni marufuku kwa mtu yeoyote kuvuna miti katika msitu ambao umehifadhiwa kwa ajili ya viumbe malum ambao ni rasilimali kwa Taifa.

- Wajibu wa
kupanda
miti
16. Kila mkazi wa Halmashauri atawajibika kupanda na kutunza miti katika eneo lake kama atakavyo elekezwa na Halmashauri.

SEHEMU YA SITA:
TAKA NGUMU NA LAINI

- Utupaji wa
taka ngumu
na laini
17. (1) Itakuwa ni wajibu wa kila Mtu ndani ya Halmashauri kuwa na shimo au chombo kwa ajili ya kutupa taka ngumu na laini na kusimamia kwa karibu usafi katika eneo lake.

(2) Mtu yeoyote atakayetupa taka ngumu au laini, kujisaidia katika miti, ziwa, mabwawa au kwenye vyanzo vyaya maji vilivyoko katika Halmashauri atakuwa ametenda kosa.

- Uendeshaji
wa viwanda
18. Itakuwa ni marufuku kuendesha shughuli za karakana, mashine ya kusaga, kuranda mbao, kukamua maji ya matunda, kuchomelea vyuma au kuendesha shughuli yoyote inayozalisha uchafu ambao unaleta athari kwa binadamu na viumbe wengine katika maeneo ya makazi ya watu bila kuzingatia taratibu za ujenzi.

SEHEMU YA SABA:
MAKOSA NA ADHABU

Sheria Ndogo Za (Hifadhi ya Mazingira) Za Halmashauri ya Mji wa Kondoa
Tangazo la Serikali Na. 512 (Linaendelea.)

- Makosa 19. Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa endapo;
- (a) ataingiza mifugo katika eneo la Halmashauri bila kibali;
 - (b) atasafirisha mifugo katika eneo la Halmashauri bila kibali;
 - (c) atasafirisha mifugo katika maeneo yasiyo ruhusiwa;
 - (d) atafuga mifugo zaidi ya idadi iliyo ruhusiwa;
 - (e) atakiuka masharti ya kilimo, kuchimba mchanga, kokoto, madini katika maeneo yasiyo ruhusiwa;
 - (f) atakiuka masharti ya kuhifadhi ardhi;
 - (g) ataharibu vyanzo vya maji au kushindwa kushiriki katika shughuli za kuhifadhi vyanzo vya maji;
 - (h) atabainika kuwa ameweka sumu ya aina yoyote kwa namna yoyote ambayo inaathiri maisha ya binadamu na viumbe wengine;
 - (i) attachoma au kusababisha moto katika misitu;
 - (j) atashindwa kushiriki katika kuzima moto;
 - (k) atavuna mazao ya misitu bila kibali;
 - (l) attachoma mkaa na kukata kuni bila kibali;
 - (m) atatupa hovyo taka ngumu au laini katika maeneo yasiyo ruhusiwa;
 - (n) atatiririsha maji machafu yanayoleta madhara kwa binadamu na viumbe vingine hai;
 - (o) ataendesha shughuli za kiwanda au viwanda vidogo, karakana, mashine za kusaga na kukoboa nafaka mashine za kuranda mbao katika makazi ya watu bila kuzingatia taratibu za mipango miji.
- Kufifilisha
kosa 20. Mkurugenzi anaweza kumtoza mtu yeyote faini isiyozidi shilingi laki tatu (Tsh.300,000/=) iwapo mkosaji atakiri kosa kwa maandishi na kuwa tayari kujaza fomu maalumu iliyoambatanishwa kwenye jedwali la Sheria Ndogo hizi na atatakiwa kulipa faini hiyo kwa mujibu wa Sheria
- Adhabu 21. Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti ya Sheria

Sheria Ndogo Za (Hifadhi ya Mazingira) Za Halmashauri ya Mji wa Kondoa
Tangazo la Serikali Na. 512 (Linaendelea.)

Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi Shilingi elfu hamsini (Tshs 50,000/=) au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili au vyote kwa pamoja yaani faini na kifungo.

JEDWALI

HATI YA KUFIFILISHA KOSA

(*Limetungwa chini ya Kifungu cha 20*)

Mimi nakiri kwa hiari
yangu mwenyewe mbele ya ambaye ni
Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Kondoza kwamba mnamo tareheya
mwezi Mwaka nilitenda kosa la kukiuka masharti ya
kifungu cha cha Sheria Ndogo za (Hifadhi ya Mazingira) za Halmashauri
ya Mji Kondoza za Mwaka 2018.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri niko tayari kulipa kiasi
cha shilingi laki tatu (Tsh 300,000/=) kama faini ninaodaiwa.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA
NIMEYATOA KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tareheya MweziMwaka

Jina:

Saini:

Mbele ya:

15 Agosti, 2018
DOODMA,

*Waziri wa Nchi-OR-TAMISEMI
SELEMANI S. JAFO (MB.),*

NAKUBALI,

*Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa
Mwenyekeji
HAMZA MAFTA*



*Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa
Mkurugenzi wa Mji
KHALIFA KONDO*

Nembo ya Halmashauri ya Mji wa kondoa imebandikwa kwenye Sheria
Ndogo hizi kufuatia azimio lilitopishwa kwenye Mkutano wa Halmashauri
uliofanika tarehe 13/5/2017 mbele ya:-

Tarehe:

Saini:

Cheo:

*Tangazo la Serikali Na. 512 (Linendeleta.)
Sheria Ndogo Za (Hiyadhi ya Mazingira) Za Halmashauri ya Mji wa Kondoa*